OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGOMA-UJIJI
SHULE YA SEKONDARI GUNGU

SHULE YA SEKONDARI GUNGU,
S.L.P 37,
KIGOMA.
Mobile No. 0754627501/
Tarehe…………………

MZAZI/MLEZI WA ……………………………………………..
YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021

1. 0. UTANGULIZI
   Ninayo furaha kukutaarifu kwamba mwanao ……………………………… amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2021 katika shule hii. Shule ya sekondari Gungu ipo katika Manispaa ya Kigoma/Ujiji, kata ya Gungu.

   Mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 25/01/2021 kama hataripoti ndani ya muda huo hatua kali za kisheria zitachukuliwa. Hivyo ni wajibu wa mzazi/mlezi kuhakikisha mwanafunzi anaripoti shule kwa wakati.

2. 0. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA
   2.1. SARE ZA SHULE

   i. Wavulana
      - ✓ Suruali mbili za rangi ya damu ya mzee, tai mbili(kitambaa cha suruali) na mashati mawili meupe mikono mifupi (Suruali ziwe pana zenye rinda mbili. Modal au suruali za kubana haziruhusiwi)
      - ✓ Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba.
      - ✓ Soksi nyeusi
      - ✓ Mkanda mweusi wa ngozi
      - ✓ Sweta rangi ya damu ya mzee.

   ii. Wasichana
      - ✓ Sketi mbili za rangi ya damu ya mzee ndefu zenye kuvuka magoti.
      - ✓ Mashati mawili meupe mikono mifupi na tai mbili (kitambaa cha sketi)
      - ✓ Hijabu zianazoruhusiwa ni kwa mujibu wa maelekezo ya dini ya kiislamu. Shati lazima liwe la mikono mirefu kwa watakaovaa hijabu. Vilemba, mitandio na hijabu fupi haviruhusiwi.
      - ✓ Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba.
      - ✓ Soksi nyeupe
      - ✓ Sweta rangi ya mzee

   2.2. VIFAA VYA MASOMO
   - ✓ Madaftari 12 (counter book quire 3)
   - ✓ Dictionary kubwa 1
   - ✓ Vitabu vya sanaa, kalamu za kutosha, rula na mkebe wa hisabati.
   - ✓ Begi la kubebea madaftari na viatbu (ni laziama kwa kila mwanafunzi).
   - ✓ Mahitaji mengine ya kibinadamu pamoja na vifaa vya usafi.
   - ✓ Huduma za matibabu na usafiri pale mwanafunzi anapougua akiwa kwenye mazingira ya shule ni jukumu la mzazi. Shule itatoa huduma ya kwanza tu pale mwanafunzi atakapozidiwa akiwa shuleni.

## 3.0. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sharia ya elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Rais TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani nan je ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
d) Kuwahi katika shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na;
h) Kutunza mali za shule.

## 4.0. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE

a) Wizi
b) Uasherati
c) Ubakaji
d) Ulevi na matumizi ya dawa za kulevya, kama vile uvutaji sigara, bangi, cocaine, mirungi, kubeli n.k
e) Kupigana au kupiga
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
g) Kudharau bendera ya taifa
h) Kuwa mjamzito/ kupata mimba
i) Kuoa au kuolewa
j) Kutoa mimba
k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
l) Kukataa adhabu kwa makusudi
m) Kuwa na simu ya mkononi

## 5.0. MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI

a) Medical Examination form amabayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
b) Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi, mkataba wa kutoshiriki migomo, fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayo tolewa na shule.

Tafadhali soma kwa makini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

Karibu sana katika shule hii na nakutakia maandalizi mema.

HEADMASTER
UNGU SEC. SCHOOL
P.O. BOX 37
KIGUMA

……………………………………..
SALUM KEAH MOHAMED
MKUU WA SHULE

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGOMA/UJIJI**

**SHULE YA SEKONDARI GUNGU**

**S.L.P 37 KIGOMA**

**MOBILE: 0754627501**

# MEDICAL EXAMINATION FORM

(To be completed by a Medical Officer in respect of all Forms One/ Five entrants)

Full Name ____________________________________________________________

Age __________________________________________________________________

Blood count (Red and White) _______________________________________________

Stool examination _______________________________________________________

Urine analysis __________________________________________________________

Syphilis test ____________________________________________________________

T.B test ________________________________________________________________

Ears ___________________________________________________________________

Eyes ___________________________________________________________________

Chest __________________________________________________________________

Spleen _________________________________________________________________

Abdomen _______________________________________________________________

ADDITIONAL INFORMATION e.g physical defects or impairments, infection chronic of family diseases

______________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________

________________________________________________________

I certify that the above is fit to pursue as stated above

Date ______________ signature __________________ designation ______________ station _________

**Note**: medical officer, At the time of examination please examine the individual for any illness you note.

NB: This form should be returned to the school with your acceptance. No any pupil/ student will be enrolled without the certificate of physical fitness.